



**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Wizara ya Mambo ya Katiba na Sheria**



WAKALA WA USAJILI UFILISI NA UDHAMINI

(RITA)

**TAARIFA YA HALI YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA USAJILI WA
WATOTO WALIO NA UMRI CHINI YA MIAKA MITANO KATIKA MIKOA
YA GEITA NA SHINYANGA.**

(21 MACHI 2017 – 21 APRILI 2017)

UTANGULIZI

Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini (RITA) ulizindua Mpango mpya wa Usajili na kutoa Vyeti vya kuzaliwa kwa Watoto walio na Umri chini ya Miaka Mitano katika Mikoa ya Geita na Shinyanga tarehe 21 Machi 2017. Lengo la mpango huu mpya ambao ni wa kudumu ni kuboresha hali ya usajili kwa kundi hilo la watoto. Kabla ya kuanza mpango huo, watoto chini ya asilimia 10 tu ndio walikuwa wamesajiliwa na kupata vyeti vya kuzaliwa katika mikoa yote miwili.

Katika utekelezaji wa mpango huu, huduma za usajili zimesogezwa karibu na maeneo ya makazi ya wananchi ambapo huduma zinapatikana BURE/BILA MALIPO katika Ofisi za Watendaji Kata na Katika Vituo vya Tiba vyote katika Mikoa hiyo.

Mpango huu vilevile unaendelea kutekelezwa katika mikoa ya Mbeya, Songwe, Mwanza, Iringa na Njombe. Taarifa hii fupi ina lengo la kutoa picha ya hali ya utekelezaji ya Mpango huu katika Mikoa ya Geita na Shinyanga kwa kipindi cha mwezi mmoja baada ya kuzinduliwa.

HALI YA UTEKELEZAJI

Usajili unaendelea katika vituo vyote vya usajili kupitia Wasajili wasaidizi ambao ni Watendaji Kata na Wahudumu wa Vituo vya Tiba waliopewa mafunzo ya kina kuhusu masuala ya Usajili wa Vizazi na Vifo. Mpango huu unatekelezwa katika Halmashauri zote 5 za mkoa Wa Shinyanga ambako kuna jumla ya vituo 322 na Halmashauri 6 za Mkoa wa Geita ilio na vituo 257.

Mpaka sasa jumla ya watoto 479,146 wamesajiliwa na kupewa vyeti vya kuzaliwa ambapo kati ya hao watoto 230151 wamesajiliwa katika Mkoa wa Shinyanga ambao ni sawa na asilimia 71 ya lengo na Mkoa wa Geita 249,000 ambao ni asilimia 60 ya watoto wote wasio na vyeti vya kuzaliwa.

Kwa Mkoa wa Shinyanga, Halmashauri ya Mji Kahama ndio inaongoza kwa kusajili asilimia 78 ya watoto na katika Mkoa huo Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga imesajili asilimia 65 ambacho ni kiwango cha chini zaidi mpaka sasa. Kwa Mkoa wa Geita, Halmashauri ya Nyangwale ndiyo inaongoza kwa kusajili asilimia 69 ya lengo ikifuatiwa na halmashauri ya Mji Geita asilimia 67. Halmashauri ya Wilaya ya Geita imesajili asilimia 56 ambayo ndio iliyo na kiwango kidogo zaidi cha usajili.

Utekelezaji unaoendelea una sehemu kuu mbili ambazo ni kampeni ya muda maalumu iliyo na lengo la kuwasajili watoto wote ambao hawana vyeti vya kuzaliwa na baada ya hapo usajili kuendelea katika vituo hivyo ili kumsajili kila mtoto anayezaliwa ili kuepuka mlundikano wa watoto wasio na vyeti vya kuzaliwa.

HITIMISHO

Lengo lililowekwa na kila mkoa ni kusajili watoto wote (asilimia 100) na kuwapa vyeti vya kuzaliwa ndani ya kipindi cha Miezi Sita. Kutokana na takwimu zilizooneshwa hapo juu ni dhahiri kwamba zoezi linaendelea vizuri kwani kila mkoa tayari umeshasajili zaidi ya nusu ya watoto kwa kipindi cha mwezi mmoja. Hii imetokana na mwamko mkubwa walionao wananchi wa kuwasajili watoto ili wapate vyeti vya kuzaliwa na usimamizi mzuri wa Viongozi katika ngazi za Mikoa, Wilaya na Halmashauri.

Natoa rai kwa wananchi wote wanaoishi katika Mikoa ya Geita na Shinyanga ambao wana watoto walio na Umri chini ya Miaka Mitano na bado hawajasajiliwa kutumia fursa hii ili kuwapatia watoto haki yao ya msingi ya kutambuliwa na kupata cheti cha kuzaliwa ambayo ni nyaraka muhimu itakayomsaidia mtoto kupata huduma nyingine nyingi za kijamii. Wananchi wakumbuke cheti kinachotolewa ni cheti cha kudumu ambacho mtoto atakitumia hata baada ya kufikisha miaka mitano.



Emmy K. Hudson
Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu

21 April 2017